

Haki za Waislamu Wenzako

341. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w. katika Bihar al- Anwar , J. 75, Uk. 150:**

“Yeyote yule anayemhuzunisha Mwislamu mwenzake basi kamwe hawezi kumfidia hata kama atamlipa dunia nzima kwani haitatosha (ispokuwa iwapo atatubu na kumfurahisha Mwislamu huyo).”

342. **Al-Imam Musa al-Kadhim a.s. Amesema katika Bihar al- Anwar, J. 2, Uk. 75:**

“Moja ya faradhi miongoni mwenu kuelekea Mwislamu mwenzenu ni kutokumficha kitu chochote ambacho kinaweza kumfaidisha humu duniani au Aakhera.”

343. **Al-Imam Al-Hassan Al Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s.**

“Watendee watu vile utakavyopenda wewe kutendewa.”

344. **Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. Amesema katika Ghurarul-Hikam, Uk. 181:**

“Alla swt humrehemu mtu ambaye anahuisha yaliyo haki na kuangamiza na kuteketeza yale yaliyo batili, au hukanusha dhuluma na kuimarisha uadilifu.”

345. **Amesema Al-Imam Ja’far as-Sadiq a.s. katika Tuhfatul-Uqul, Uk. 277:**

“Tabia hizi nne ni kutokea tabia za Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w: haki, ukarimu, subira na kuvumilia katika shida, na kusimamia haki ya Mumiin.”

346. **Al Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s. Amesema katika Nahjul-Balagha, Barua na 53:**

“Kwa hakika ni watu wa kawaida ndio walio nguzo za Dini, nguvu ya Waislamu na hifadhi dhidi ya maadui. Hivyo mwelekeo wako daima uwe kuelekea wao na uwanyenyekee.”

347. **Amesema Al-Imam Ja’far as-Sadiq a.s. katika Al-Kafi, J. 2, Uk. 170:**

“Allah swt haabudiwi zaidi ya thamani kuliko kutimiza haki ya Mumiin.”

348. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w katika Bihar al- Anwar, J. 67, Uk. 72:**

“Yeyote yule anayemuudhi Mumiin, basi ameniudhi mimi.”

349. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w katika Mustadrak al-Was’iil, J. 17, Uk. 89:**

“Yeyote yule atakayemdhulumu Muumin mali yake pasi na hakie, basi Allah swt ataendelea kumghadhibikia na wala hatazikubali matendo yake mema atakayokuwa akiyatenda; na hakuna hata mema moja itakayoandikwa katika hisabu zake nzuri hadi hapo yeye atakapofanya tawba na kuirudisha hiyo mali kwa mwenyewe.”

Source URL: <https://www.al-islam.org/node/24379>